JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**

Idara Kuu ya Utumishi,
S.L.P. 2483, DAR ES SALAAM
Simu ya Upepo; Simu: 118531I/4,
Fax.: 113084, 131365

Unapojibu tafadhali taja:

*Kumb. Na. C/AB/10/48/01/92* 29 Julai, 1999

## WARAKA WA UTUMISHI NAMBA 1 WA MWAKA 1999 UTARATIBU WA UHAMISHO WA WATUMISHI KUTOKA SERIKALI KUU KWENDA KWENYE WAKALA WA SERIKALI

**1.0 Utangulizi:**

1.1 Wakala wa Serikali zimeanzishwa kwa sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 (The Executive Agencies Act, 1997) kama vyombo vya utekelezaji kwa niaba na chini ya uangalizi wa Serikali. Kila Wakala utakuwa na mfumo unaoonyesha utekelezaji wa majukumu yaliyokuwa yanafanywa na idara za Serikali kwa ufanisi zaidi.

1.2 Nia ya Waraka huu ni kutoa maelekezo ya utaratibu utakaofuatwa katika kuhamisha watumishi kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Wakala wa Serikali. Pia ni nia ya Waraka kutoa maelekezo ya taratibu zitakazohusu hatima ya watumishi watakaokosa nafasi za kazi katika Wakala wa Serikali.

**2.0 Uhamisho wa kuazimwa (Secondment) na Masharti yake:**

2.1 Watumishi wa Serikali watakaojiunga na Wakala wa Serikali wakati wa uanzilishi kutokana na idara zao kugeuzwa kuwa Wakala watakwenda huko kwa uhamisho wa moja kwa moja. Hata hivyo italazimu watumishi hao wawe na muda wa majaribio wa miezi kumi na miwili (12) utakaowawezesha pande zote mbili mwajiri (Wakala) na mtumishi kufanya maamuzi ya kuendeleza ajira au vinginevyo. Ni kwa ajili hiyo mwaka wa kwanza utahesabika kuwa kipindi cha kuazimwa. Wakati wa kipindi cha kuazimwa Wakala itawalipa watumishi hao mishahara na maslahi mengine.

2.2 Watumishi watakaoshindwa kuendelea na ajira ya moja kwa moja kwenye Wakala katika kipindi cha majaribio watarejeshwa kwenye Wizara mama ambako wataendelea na ajira zao kama nafasi zao zitakuwepo, na endapo nafasi za ajira zitakosekana, itabidi wastaafishwe kwa kuzingatia kanuni na taratibu zinazotawala zoezi la kupunguza watumishi wa Serikali.

2.3 Aidha inasisitizwa kwamba uhamisho wa kuazimwa utazingatia masharti yaliyofafanuliwa katika kifungu Q.45 cha Kanuni za Kudumu (Standing Orders), Toleo la II, 1994.

**3.0 Uhamisho wa moja kwa moja (Permanent Transfer) na Masharti yake:**

3.1 Uhamisho wa moja kwa moja kutoka Serikalini kwenda kwenye Wakala wa Serikali utafanyika baada ya mtumishi aliyeazimwa kumaliza muda wa kuazimwa kama ilivyoelezwa katika ibara ya 2.1 hapo juu. Inasisitizwa kwamba baada ya watumishi kuhamia moja kwa moja kwenye Wakala wa Serikali Wizara mama zitafuta ikama zao.

3.2 Uhamisho wa mtumishi kutoka Serikali kwenda katika Wakala wa Serikali, au kurudi/kwenda, katika Serikali utafanyika kwa makubaliano kati ya mtumishi wa Wakala, na utaidhinishwa na Katibu Mkuu wa Idara Kuu ya Utumishi Serikalini (Permanent Secretary - Establishments).

3.3 Mbali na watumishi watakaohamishiwa kwenye Wakala wa Serikali kwa utaratibu wa kuazimwa au uhamisho wa moja kwa moja, pia watakuwepo watumishi watakaoshikizwa (attachment) kwenye Wakala. Utaratibu wa kushikizwa utazingatia ufafanuzi ulio katika ibara ya 4 ya Waraka wa Utumishi Na. 9 wa mwaka 1992. Mtumishi anayeshikizwa kwenye Wakala wa Serikali ataendelea kuwa mtumishi wa mwajiri wake (alikotoka) na siyo alikoshikizwa au kuazimwa. Iwapo mshahara wa cheo, atakachoshikizwa ni mkubwa kuliko ule wa mwajiri wake wa mwanzo, mwajiri mpya wa mahali alikoshikizwa atamlipa tofauti ya mshahara.

3.4 Mtumishi anayehamishwa moja kwa moja kutoka Serikali Kuu kwenda katika Wakala wa Serikali atalipwa mshahara wa cheo cha nafasi ya ajira atakayopewa katika wakala alikohamia. Kama mshahara wa wakala utakuwa mdogo kuliko ule aliokuwa analipwa serikalini, atakuwa analipwa serikalini kama mshahara wake binafsi (personal to one self), isipokuwa kama mtumishi mwingine atahiari kuajiriwa kwenye kazi yenye mshahara mdogo zaidi.

3.5 Inasisitizwa kuwa kwa watumishi wote wa wakala wa serikali, iwe ni kwa kuazimwa, uhamisho wa moja kwa moja au kushikizwa, mamlaka ya nidhamu ni wakala wa serikali husika.

**4.0 Pensheni:**

4.1 Hakutakuwa na mabadiliko katika taratibu za pensheni kwa watumishi wa Serikali wanaoazimwa au kuhamia kwenye Wakala wa Serikali. Malipo ya pensheni yatalipwa kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa katika Tangazo la Serikali Na. 75 la tarehe 19 Machi, 1999 (Govern-ment Notice No. 75 of March 19, 1999) na Executive Agencies (Per-sonnel Management) Regulations, kifungu 40, kinachoelekeza kama ifuatavyo:-

40.-(l) Until other arrangements are made, superannuation arrangements for persons who on the date on which the agency in which he is employed is established shall be those applicable to him immediately before that date.

(2) Nothing in these regulations shall be construed as prohibiting the employment of any person to whom paragraph (1) applies on contract terms.

(3) In these regulations, "superannuations arrangements" means pen-sions or provident fund or any other security arrangement".

4.2 Aidha, kifungu cha 2 cha Sheria ya Pensheni kwa Watumishi wa Umma Na. 2 ya mwaka 1999 (Public Service Retirement Benefits Act, 1999) kinatamka kwamba sheria hiyo inawahusu watumishi wa Serikali pamoja na Wakala wa Serikali, kwa hiyo masharti ya pensheni chini ya sheria hiyo yanawahusu pia watumishi wa Wakala wa Serikali.

**5.0 Tarehe ya kuanza kutumika:**

Waraka huu unaanza kutumika kuanzia tarehe 19 Machi, 1999.

J. A. RUGUMYAMHETO,

*Katibu Mkuu (Utumishi)*